JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA TATU

**21 APRILI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 21 APRILI, 2016

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI MKUU:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## II. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**21. MHESHIMIWA EZEKIEL MAGOLYO MAIGE (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mvua ya Theluji iliyonyesha tarehe 3 Machi, 2015 ilisababisha maafa makubwa ambapo familia 650 zilikosa makazi na Mheshimiwa Rais wakati huo aliwaahidi wahanga wa maafa hayo kuwa Serikali itasaidia kujenga nyumba 343:-

(a) Je, ni nyumba ngapi hadi sasa zimejengwa katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais;

(b) Je, ni kiasi gani cha pesa kimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi hiyo;

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha na misaada ya kibinadamu ya aina nyingine iliyotolewa na Serikali katika kukabiliana na janga hilo.

**22. MHESHIMIWA HALIMA ABDALLAH BULEMBO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Nchi ya Tanzania ni moja kati ya nchi zenye vijana wengi, asilimia 72 ya Watanzania wapo kwenye umri chini ya miaka 29 kwa mujibu wa Ofisi ya Takwimu ya Taifa 2013 na Ajira kwa Vijana hao ndiyo suluhisho la kuhakikisha kuwa vijana wanalihudumia Taifa lao:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwawezesha vijana wawe wajasiriamali kwa kuwapa mitaji, mikopo na ni vigezo gani vitakavyosimamia na kuwalinda na kuweka usawa wa upatikanaji wa ushiriki wao katika fursa hizo;

(b) Je, ni lini ahadi ya Tsh. 50,000,000/= kwa kila kijiji itatekelezwa na vijana watapata mgao wa asilimia ngapi kutoka fungu hilo.

**23. MHESHIMIWA YUSSUF SALIM HUSSEIN (CHAMBANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kuna idadi kubwa ya vijana wa Tanzania ambao wanafanya kazi nje ya nchi zikiwemo kazi za ndani (House girls):-

(a) Je, ni utaratibu gani unatumika kwa vijana hao kwenda kufanya kazi hizo nje ya nchi;

(b) Je, ni vijana wangapi wanaofanya kazi hizo nje ya nchi.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI)**:-

**24. MHESHIMIWA MUSUKUMA JOSEPH KASHEKU (GEITA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Geita imefanywa kuwa hospitali ya Mkoa tangu tarehe 8/1/2016:-

Je, ni lini DMO aliyekuwa akiongoza hospitali hiyo atahamia katika hospitali iliyopendekezwa na kikao cha RCC kuwa hospitali ya Wilaya.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

### 25. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi Na Utawala Bora): Mwaka 2002 Serikali ilipitisha Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 na marekebisho yake ya mwaka 2008 yaliyoweka mfumo wa wazi wa upimaji na ujazaji wa mkataba wa utendaji kazi (OPRAS):-

(a) Je, ni kwa kiasi gani mfumo huo umetekelezwa nchini;

(b) Je, ni lini mfumo wa kupima taasisi (*Institutional Performance*) utaanzishwa na kuanza kutangazwa hadharani.

## WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

### 26. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Hivi karibuni Jimbo la Kigamboni limetangazwa kuwa Wilaya mpya, hata hivyo Wananchi wake bado wanapata huduma ya Mahakama kupitia Wilaya ya Temeke:-

(a) Je, Serikali itaanzisha lini Mahakama ya Wilaya ya Kigamboni;

(b) Je, utekelezaji wa hatua hiyo utaanza lini.

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**27. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:-

Je, ni lini Serikali itafungua rasmi kiwanda cha kutengeneza matairi cha "General Tyre" ambacho kilikuwa ni Mkombozi mkubwa kwa uchumi wa Taifa na Ajira kwa Wananchi wa Arusha.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**28. MHESHIMIWA MARY DEO MURO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, ni kwa nini Mkoa wa Pwani usiwe na mamlaka yake ya maji kuliko ilivyo sasa kuwa chini ya DAWASCO ambapo hakuna huduma ya uondoaji maji machafu na bei ya maji iko juu kuliko ile ya Dar es Salaam.

## WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:

### 29. MHESHIMIWA DANIEL NICODEMUS NSANZUGWANKO (KASULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo:- Mkoa wa Kigoma unaongoza kwa kuwa na vijana wengi wanamichezo na wasanii mfano Shaban Robert, Diamond, Ali Kiba, Banana Zoro, Linex, Mrisho Mpoto n.k.:-

(a) Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika Mkoa wa Kigoma kwa kujenga jumba la sanaa (*Theatre Centre*) ili vijana hawa wawe na sehemu nzuri ya kuendesha shughuli zao;

(b) Kama Serikali inakubaliana na hoja hiyo kituo hicho kitaanza kujengwa lini.

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

### 30. MHESHIMIWA CONCHESTER LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Katika Bajeti ya mwaka 2015/16 Serikali kupitia Waziri wa Fedha iliahidi kupandisha pensheni kwa wastaafu wanaolipwa Tshs. 50,000 ili walipwe Tshs. 100,000/=:-

Je, Serikali imetekeleza ahadi hiyo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa lijadili na kuidhinisha Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2017 – 2020/2021.

***(majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**21 APRILI, 2016** **KATIBU WA BUNGE**